JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Namba za simu
Mkuu wa shule: 0765842864

Shule yaSekondari Kantalamba,
S.L.P. 70, Simu 025-2802017
SUMBAWANGA.

TAREHE : ……

MWANAFUNZI ……

S.L.P. ……

…….....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE HII MWAKA 2023.

Ninayo furaha kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kantalamba katika kidato cha kwanza (FI) mwaka 2023. Ninachukua nafasi hii kukupongeza kwa jitihada zako zilizowezesha kustahili uchaguzi huu. Nitegemeo langu kwamba jitihada hizo utaziongeza uwapo katika shule hii. Shule ya Sekondari Kantalamba ipo katika Manispaa ya Sumbawanga. Manispaa hii ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa, ipo umbali wa kilometa 336 toka Mbeya na kilometa 240 toka Mpanda. Upo usafiri wa uhakika kila siku toka Mbeya ambapo mabasi huanza huondoka kuanzia saa 12:00 alfajiri na kuwasili Sumbawanga saa 6:00 mchana. Kutoka Mpanda usafiri upo kila siku ambapo magari huanza kuondoka saa 12:00 asubuhi na kuwasili Sumbawanga saa 4:00 mchana. Shule ipo umbali wa kilometa tatu (3) toka Makao Makuu ya mkoa. Kwa kutumia usafiri wa pikipiki utalipa shs.1,000/= tu na kwa kutumia bajaji utalipa Tshs 700/= tu. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 09/01/2023. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia 07/01/2023 na mwisho wa kuripoti ni 20/01/2023.

Yafuatayo ni maagizo na mahitaji muhimu ambayo utatakiwa kuyatimiza kabla ya kujiunga na shule hii.

MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA

A: SARE YA SHULE

i. **SURUALI 1 DARK BLUE**: Yenye marinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (tunup) na isiyo **bana chini**.

ii. **SURUALI 1 KAKI:** Yenye marinda mawili kila upande na mkunjo au pindochini (tunup) na isiyo **bana chini**.

iii. **SURUALI 1 NYEUSI**: Yenye marinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (tunup) na isiyo **bana chini**.
NB: Suruali zote zinapatikana shuleni ili kuepuka kutofautiana rangi.

iv. **SHATI 2 ZA RANGI NYEUPE**: Mikono mirefu lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto.

v. **TAI**: Rangi dark blue na kaki.

vi. **VIATU**:
- ❖ Rangi nyeusi vyenye kamba, visiwe na soli nene, hairuhusiwi kuvaa viatu vya matairi,
- ❖ Kandambili au yeboyebo wakati wa masomo darasani na bwaloni/ukumbi wa chakula haviruhusiwi.

(vi) **SOKSI:**

- ❖ Rangi nyeupe isiyo na urembo wowote

(vii) **MKANDA:**

- ❖ Rangi nyeusi na uwe wa ngozi
- ❖ Usiwe na madoa au urembo wowote

(viii) **T.SHIRTS:**

- ❖ T.shirtmbili (2). Moja kwa ajili ya darasani na nyingine kwa ajili ya kushindia
- ❖ Rangi ya bluu yenye kola na yenye nembo ya shule.

NB. T.shirts zote zinapatikana shuleni ili kuepuka kutofautiana kwa rangi za sare hii ikiwa ni pamoja na kuwa na nembo ya shule na maandishi. Kila T.shirt ni shilingi 13,000/=

(ix) **SWETA:** Rangi ya blue

(xi) **NGUO ZA MICHEZO**

- ❖ Unatakiwa uje na nguo za michezo ambazoni bukta na fulana zote rangi ya bluu na track suit rangi nyeusi.(Nguo zote za michezo zisiwe na maandishi ya ushabiki wa timu yoyote- ndani na nje ya nchi).
- ❖ Uje na Raba kwa ajili ya michezo.

(xii) **NGUO ZA KUSHINDIA**

- ❖ Nguo za kushindia ni suruali nyeusi na T-shirt rangi ya blue kama ilivyoelekezwa hapo juu.
- ❖ Hairuhusiwi kuja na nguo za nyumbani.

B. VYOMBO VYA CHAKULA

- ❖ Nunua vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe pamoja na kijiko.

C. VIFAA VYA USAFI

Uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi:-

i. Mifagio miwili (2) aina ya chelewa kwa ajli ya usafi wa mazingira
ii. Jembe lenye mpini.
iii. Mopa/Drier 1 (Rubber squeezer)
iv. Reki 1
v. Uje na ndoo tatu (3) za lita 10 kwa ajili ya (i) kuchotea maji ya jikoni, (ii) kusafisha chooni, (iii) usafi binafsi.
vi. Fyekeo 1.
vii. Sink brush (Brashi ya kusafishia chooni.- Wanafunzi wanatumia vyoo vya maji).

NB: VILETWE VIFAA NA SI PESA PESA HAZITAPOKELEWA.

D. RIM

Rimu mbili (2) Za karatasi kwa ajili ya mitihani ya mara kwa mara. Ikiwa ni rimu moja kwa kila muhula. (ZILETWE RIMU NA SI PESA.PESA HAZITAPOKELEWA).

E. MAHITAJI MENGINE

a) Godoro futi 2½

b) Chandarua, mashuka mawili blue bahari

c) Taulo, blanketi na Sanduku la chuma (original)

d) Nakala ngumu (Hard Copy) ya cheti cha kuzaliwa usilete Cheti Halisi (Original Birth Certificate).

F. MAHITAJI YA KITAALUMA

a) Madaftari ya kutosha (counter books 11)

b) Vitabu vya masomo ya:-

i. Physics
ii. Chemistry
iii. History
iv. Geography
v. Mathematics
vi. Civics
vii. Kiswahili
viii. Biology
ix. Agriculture
x. Physical Education
xi. English Language
xii. Elimu ya Dini ya Kiislamu (kwa waislamu).
xiii. Mkebe wa somo la hisabati (Mathematical set)
xiv. Kalamu za kutosha na Penseli
xv. Rula mbili
xvi. Vifutio.

G. FEDHA ZA MATIBABU NA MATUMIZI.

a) Unashauriwa uje na fedha ya matumizi madogo madogo kama vile kununua sabuni, mafuta n.k.

b) Unashauliwa kumkatia bima ya afya mwanao (NHIF) au uje na Tshs 50,400/= ambazo mara baada ya kumsajili kwenye mfumo utaenda mwenyewe ukiongozana na muuguzi wa shule kukata BIMA YA AFYA.TAKWA ILI NI LA KISHERIA.Utakiwi kupuuzia.

H. LIKIZO ZA MIHULA.

Mwezi wa Juni na Disemba hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kubaki shuleni wakati wa likizo.

I. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi na yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulinga na ratiba ya shule ni lazima.

iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
ix. Kutunza mali za umma

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Uasherati na ushoga
iv. Ubakaji
v. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
vi. Kupigana au kupiga
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
viii. Kudharau Bendera yaTaifa
ix. Kumpa mimba mwanafunzi
x. Kuoa au kuolewa
xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvunja amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kushiriki kutoa mimba
xiii. Kufuga ndevu
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na vyumba vya kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa, kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu, n.k.
xvii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
xviii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi.

NB.*Unaruhusiwa kusafiri na simu ili kurahisisha mawasiliano ukiwa njiani.Lakini unapofika shuleni tu siku hiyo ukabidhi simu kwa makamu mkuu wa shule au mwalimu wa zamu.Kama wote hawapo ukabidhi kwa mwalimu yeyote aliyeko shuleni. Ukikamatwa na simu adhabu yake ni KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA.*

……..
LEONSIUS MBELWA WILLIAM
MKUU WA SHULE.
PRIME MINISTER'S OFFICE- REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.

KANTALAMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 70,
SUMBAWANGA

DATE.....

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL
.....
.....

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A.

Name .....

Please examine the above named as to HIS/HER physical and mental fitness as indicate below and arrange for necessary treatment if required. This certificate must be signed by qualified medical officer of a government Hospital and returned to school by the student.

The examination should include the following categories:

1. Sight
2. Hearing
3. Hemoglobin
4. Blood pressure
5. Pulmonary tuberculosis
6. Neurosis
7. Venereal diseases
8. Skin diseases
9. Urine
10. Leprosy
11. Any disability
12. Stool
13. Pregnancies test
14. Other serious disease

PART B :

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named student and consider that she /he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full schooling.
2. Other comments.....

Date ..... Signature and Official stamp